**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**

# TAARIFA KWA UMMA

## MATOKEO YA MTIHANI WA USAJILI NA LESENI ULIOFANYIKA TAREHE 23.08.2024

**07.11.2024, Dodoma**

Napenda kuwajulisha kuwa matokeo ya Mtihani wa usajili na leseni uliofanyika tarehe **23 Agosti, 2024** yametolewa leo tarehe **07 Novemba, 2024** baada ya kukamilisha mchakato wa taratibu za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania ya mwaka 2010 ***(The Nursing and Midwifery Act.2010).***

Matokeo haya yametolewa kupitia akaunti ya mtahiniwa iliyopo kwenye mfumo wa kumbukumbu wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMCIS). Hivyo, kila mtahiniwa atembelee akaunti yake katika mfumo wa Baraza **https://tnmcis.tnmc.go.tz.** na kuweza kuona matokeo yake.

Kwa ambao wameshindwa Mtihani huu, wanajulishwa kuwa tarehe ya kurudia mtihani kwa kipindi kingine itakuwa tarehe **20 Desemba, 2024**. Taratibu za maombi zimeelekezwa katika tovuti ya Baraza.

Aidha, Baraza **linaomba radhi kwa** kuchelewa kutoa matokeo haya na kwa usumbufu uliojitokeza kwa kipindi hiki cha kusubiria matokeo.

Ninawashukuru kwa ushirikiano wenu.

**Imetolewa na: -**

Agnes Mtawa

**MSAJILI-TNMC**